

**UJUMBE RASMI**

Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu Kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani 2021

## Dhamira Yetu ni Kulinda Haki na Utu wa Wafanyakazi

Taasisi ya Afya Ifakara inathamini juhudni na mapambano ya kihistoria wa wafanyakazi duniani, wakiwemo wa Taasisi yetu, ambayo lengo lake in kufanya dunia iwe mahali salama zaidi kuishi. Katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani leo hii, tunapenda kurejea dhamira yetu kuendelea kuhakikisha mustakbali bora na fursa zaidi kwa wafanyakazi wetu, hii ikiwa inaafikiana na ahadi ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) linaloelekeza "kuhakikisha kuwa haki na utu wa wafanyakazi unalindwa."

Kwa mara nyingine tena mwaka huu, tunaadhimisha Siku hii tukiwa na janga la Corona. Hivyo basi, tunapaswa kukumbushana kuhusu umuhimu wa kuchukuwa tahadhari muda wote huku tukifuata miongozo iliyopendekezwa; kufanya kazi maelekezo ya wataalamu wa afya; na kutii maelekezo yanayotolewa na mamlaka zetu. Tunapaswa kuendelea kujilinda mpaka pale tutakapohakikisha kuwa tuko salama, maana hakuna aliye salama mpaka pale wote tutakapokuwa salama.

Menejimenti ya IHI inatambua na kujivunia juhudni zinazoendelea kufanywa na nyinyi wafanyakazi na wadau wetu. Tunajali na kuheshimu kazi zenu. Na kwa namna ya pekee, tunathamini michango yetu kwenye nafasi mnazofanya kazi, tukiamini kuwa, kuititia dhamira njema iliyopo na kujitoa kwenu, mnayo nguvu ya kuibadilisha dunia na kutuwezesha kufikia lengo letu la kuboresha afya na maisha ya watu.

Tunawatachia maadhimisho mema ya Siku ya Mei Mosi!

**Dk. Honorati Masanja**

Mkurugenzi Mkuu, IHI  
Jumamosi Mei 1, 2021